# Wafugaji waoneshwa fursa ujenzi wa bomba la mafuta

**Na ALLAN KITWE,** *Igunga*

WAFUGAJI wilaya ya Igunga, mkoani Tabora, wametakiwa kuchangamkia fursa ya ujio wa mradi wa bomba la mafuta kutoka Hoima nchini Uganda hadi Chongoleani, mkoani Tanga kupitia wilayani hapa.

Rai hiyo ilitolewa juzi na Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Mji Mdogo Igunga, Joseph Sambo, alipokuwa akizungumza na gazeti hili na kueleza kuwa wafugaji wana nafasi kubwa ya kunufaika na mradi huo.

Alisema mradi huo ambao upo katika hatua za mwisho kuanza utekelezaji utapita katika ardhi ya wilaya hiyo na kujengwa moja ya vituo vya kusafishia mafuta.

Alibainisha kuwa wakati wa ujenzi wa bomba hilo, mafundi watahitaji huduma za chakula, vinywaji, kitoweo cha nyama, mayai na malazi na kuwataka wafuga kuku, mbuzi, ng'ombe na bata kukaa mkao wa kula.

"Wafugaji wetu jiandaeni kutoa huduma ya kitoweo kwa mafundi na wafanyakazi wa mradi, msiwaachie wauza kuku, mbuzi, bata na ng'ombe kutoa wilaya nyingine waje kutoa huduma hizo," alisema.

Mkurugenzi Sambo alisema ujio wa mradi huo ni fursa muhimu kwa uchumi wa wakazi wa wilaya hiyo, hivyo kila mmoja anapaswa kujiandaa ili mradi utakapoanza, huduma zote zipatikane na wajiongezee kipato.

Alitoa wito kwa wafanyabishara na watoa huduma za usafiri kujipanga vizuri ili mradi utakapoanza zitakazohitajika zipatikane.

Mtaalamu wa mifugo wa mamlaka ya mji huo, Andreas Kafuru, alisema wilaya hiyo hususan Mji wa Igunga umejaaliwa kuwa na mifugo mingi ambayo ni chanzo kizuri cha mapato ya wananchi, halmashauri na taifa.

Alifafanua kuwa mradi huo ni fursa muhimu inayoweza kunufaisha sekta ya mifugo na uvuvi kutokana na idadi kubwa ya mifugo iliyopo ambayo ni ng'ombe 687,911, mbuzi 378,951, kondoo 213,755, kuku 1,500,253 na nguruwe 62,528.

Aliongeza kuwa idara yake imeendelea kuhamasisha ufugaji wa kisasa kuimarisha na kuboresha miundombinu mfano machinjio, masoko ya mifugo na samaki na mabucha ili kuhakikisha wafugaji wananufaika zaidi.

**UHAMASISHAJI**

## UFUGAJI KISASA

Mtaalamu wa mifugo wa mamlaka ya mji huo, Andreas Kafuru, amesema idara yake imeendelea kuhamasisha ufugaji wa kisasa kuimarisha na kuboresha miundombinu mfano machinjio, masoko ya mifugo na samaki na mabucha

Scanned with CamScanner

# Prof Ngowi alivyozungumzia uchumi wa buluu

**Na Jenifer Gilla**

MWAKA mmoja uliopita, Mhadhiri wa Uchumi katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Hayati Prof. Honest Ngowi, alialikwa katika Kongamano la Uchumi wa Buluu Zanzibar, kuzungumzia fursa zinazopatikana kwenye eneo hilo.

Alisema uchumi wa buluu ni utumiaji endelevu wa rasilimali za bahari kiuchumi, ikiwamo uvuvi, kutengeneza vizimba vya kuuzia samaki, kutengeneza majokofu ya kuhifadhia samaki ili kuongeza ubora wa maisha.

Prof. Ngowi alisema kuwa uchumi wa buluu ni moja ya jukwaa lenye kuleta maendeleo ambayo ndani yake kuna mambo mengi ikiwamo viwanda, kilimo na madini ambayo huleta ajira kwa watu na kusaidia kuondoa umaskini.

Alisema jukwaa kama la uchumi wa buluu sio kitu kipya, suala la msingi la kujiuliza ni je, jamii inalitumiaje jukwaa hilo? Lisipotumiwa vizuri itakuwa ni historia tu kuwa kulikuwapo na kitu fulani katika jamii, lakini likitumiwa vizuri inakuwa ni hazina endelevu.

Alisema siku zote fursa huwa hazimfuati mtu na jamii inapaswa kuzitafuta kutoka sehemu mbalimbali, ikiwamo uchumi wa buluu na kuzitendea haki kwa maana ya kuwekeza huko ili kujiongezea kipato na kupunguza kasi ya umaskini.

Akizungumzia fursa zinazopatikana katika sekta hiyo, alisema ni pamoja na kulisha watu wanohusika na biashara ya samaki wakiwamo mama ntilie.

Alitoa mfano wa Mafya ambako shughuli za uvuvi zimeshamiri na kusema kuwa hata wale wanaohusika kuwapikia chakula wavuvi katika viwanda vya samaki wapo katika mnyororo wa uchumi wa buluu.

Fursa nyingine latika uchumi wa buluu anaitaja kuwa ni utengenezaji wa barafu za kuhifadhia samaki, ambayo barafu moja huuzwa kwa Sh. 500 hadi 2,000. Mtu akiweza kuuza dumu 10 kwa siku ana uhakika wa kuingiza Sh. 5,000 hadi 20,000.

Kilimo cha zao la mwani kinatajwa kuwa fursa nyingine kwamba kuanzia kuuza pembejeo na mbegu, kulima, kuchakata na pia kuuweka kwenye makasha (parckaging) na hata huduma za ugavi, zote ni fursa zinazoweza kumwingizia mtu kipato.

Fursa nyingine kwa mujibu wa Prof. Ngowi ni shughuli za usafirishaji wa abiria na mizigo, ikiwamo maboti na meli.

Alisema kinachoangaliwa hapo sio vyombo pekee bali hata wanaohusika kuviendesha akiwamo baharia, kapteni, biashara ya vyakula ndani za meli hizo, vyote ni uchumi wa buluu.

Alitaja suala la uvunaji wa viumbe hai waishio baharini kama samaki, ambao hutumika kwa ajili ya chakula, ambalo anahitajika mvuvi, mnunuzi, mkaangaji na mlaji.

Pia, alisema baadhi ya viumbe hao mabaki yao hutumika kutengenezea urembo kama bangili, hereni, cheni na mapambo mengine ya ukutani ambayo hufanya vizuri kwenye masoko ya kitaifa na kimataifa.

Utalii, alisema ni sehemu ya uchumi wa buluu ikiwamo fukwe kutumika kama sehemu ya kupumzikia, hoteli kubwa, vyakula vinavyolisha watalii, zote ni fursa zinazopatikana katika uchumi wa buluu.

Scanned with CamScanner

# Wafugaji wahimizwa kulima malisho

**Na John Nditi, Morogoro**

WAFUGAJI nchini wameshauriwa kulima mashamba ya malisho yanayoweza kuhimili ukame na kuhifadhi majani wakati wa masika ili yatumike kiangazi kwa mifugo yao na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi yanayoendelea kujitokeza kila mwaka.

Mkurugenzi Mtendaji wa taasisi isiyo ya kiserikali inayojishughulisha kuchochea maendeleo endelevu kupitia kutatua changamoto zinazohusiana na nishati, mabadiliko ya tabianchi na utunzaji wa Mazingira (FECE), Dk Dominico Kilemo, alitoa rai hiyo hivi karibuni kwenye mkutano wa 12 wa siku ya malisho Tanzania.

Mkutano huo ulienda sambamba na mkutano wa tano wa kisayansi ambao pia uliangalia mambo mengine yakiwemo matokeo ya tafiti mbalimbali zilizofanyika katika nyanda za malisho na kuona hatua walizofikia.

Dk Kilemo alisema mabadiliko ya tabianchi yamesababisha athari kubwa, sio kwa wafugaji peke yao bali na kwa wakulima.

"Kutokana na athari hizi ndio maana katika eneo la Kongwa mkoani Dodoma, tumeanzisha mradi wa kusaidia makundi haya kuhimili hali hiyo na tunaendelea kuwasaidia wafugaji zaidi kujifunza na kupata maarifa," alisema.

Dk Kilemo alisema wamekuwa wakiwashauri wafugaji kulima malisho yanayoweza kuhimili ukame yakiwemo aina ya bracharia, kuhifadhi majani wakati wa masika ili yatumike kiangazi, kuwapa mbinu za kuongeza kipato hata wanapoathirika na mabadiliko ya tabianchi na mbinu nyinginezo za kujikwamua kiuchumi.

Naye Katibu wa Chama cha Nyanda za Malisho Tanzania, Dk George Msallya alisema maeneo ya kulishia mifugo yamezidi kupungua na kutotosheleza idadi ya mifugo iliyopo. Alisema kumekuwa pia na uhaba wa maji kutokana na mabadiliko ya tabianchi.

Kwa upande wao, wafugaji wa Jamii ya Kimasai waliiomba serikali na wadau wengine wa maendeleo kuwaelimisha juu ya namna ya kumiliki ardhi ili kuondokana na matumizi holela ya ardhi bila ulinzi wa kisheria.

Scanned with CamScanner